## Mbinu: *Kujifunza kutokana na Mafanikio*

Kujifunza kutokana na Mafanikio ni mbinu ilikuzwa kwa kupitia Prof. Jona Rosenfeld kwa kuwafanya wafanya mazoezi (mwalimu, anafanyakazi ya ustawi wa jamii, mwanaharakati) kujifunza kwa vitendo. Orna Shemer, ni mwalimu wa chuo kikuu cha Yerusalemu ambae alijifunza mbinu hii, na alikuja Tanzania kusaidia washiriki katika semina kuangalia vitendo vyao na kujitoa kutoka njia ya mafanikio.



**Orna Shemer**

Alisema katika kuweka sawa ,kila mtu ana aina ya mafanikio katika maisha. (…) Tunajua ya kwamba mnafanya kazi pamoja, lakini tutamuuliza kila mmoja wenu: anafanya nini?... Atasema kwa mfano :'niliwaalika watoto ',ni takuliza : uliwezaje kuwaalika hao?'...Maswali yetu tuna taka kupata ujuzi wa kila mmoja wetu... Ujuzi huo unakuja kutokana na uzoefu.”

Katika njia hii, kinacholengwa ni mtu alichokifanya, badala ya dhamira au uhalalisho. Kutokana na ujuzi, baadae kundi litajaribu kutengeneza “Kanuni ya Vitendo”. Sentensi hizi kutoka vitendo mbalimbali mfano. Kanuni hizi huanza kutoka hatua rahisi (mfano: 'Kufuata mpangilio wa kanuni ya vitendo ukweli wa watoto') kujitoa kwa undani sana (mfano: 'Kupambana na ubaguzi. kuJenga amani kati ya watu').

## Nini nimejifunza?” Kujifunza kutokana na Mafanikio” kutengeneza mawazo chanya

Katika Maarifa Hatua za Kujitolea katika kituo cha Kimataifa cha ATD Dunia ya Nne yenye makao makuu yake nchini Ufaransa, sisi ujiuliza maswali kila siku: Jinsi gani wanachama wa harakati wanaweza kupata msaada wanaohitaji kuimarisha ujuzi wao wa watu wao wanahusika kuboresha hatua zao, ili iweze kuwa ukombozi na kufikia wale ambao bado wako katika umaskini. Kwahiyo inaweza kuwa kwa kujikomboa na kuwafikia wale wote waliokuwa wanakwama katka umaskini. Tulipo pata kumfahamu Orna na kazi yake' 'Kujifunza kutokana na Mafanikio', tuligundua mawazo chanya yalijengeka. Pamoja na Viongozi wa Kanda ya Africa tuliwaalika kushiriki katika semina ya vijana Dar es Salaam.

Kuja Afrika kwa mara ya kwanza na kupitia njia mpya ya kujifunza pamoja na vijana kutoka nchi mbalimbali za Afrika, njia mbalimbali za maisha, asili tofauti na uzoefu, ilikuwa kwa ajili ya Orna na mimi mwenyewe kusisimua jituhada.


Kwa kupitia semina wote, tuligundua jinsi gani kila mtu anajaribu “Kuwa na rafiki na rafiki asiyekuwa na rafiki” kwa kupitia kushirikishana muda, ujuzi, ubunifu na kuipenda kazi waliopewa na Orna kutaka kitu “cha kwanza kinakuwa kwa kuona” ili itusaidie kwa mawazo na kuona kwa macho.

Grace aliimba nyimbo na watoto nakuwafanya watoto wengi na kufanya nyimbo nying kutoka ujumbe wa watoto: tuliweza kuona Kristiani aliandaa na kuwezesha ratiba ya vipindi vya redio na watoto kwa kila wiki Tapori watoto husikiliza watoto wenzao wazazi na walimu, na wakati mwingine wanasiasa.Tulimuona Shafi aliongoza rafiki zake kuzuia uhalifu wizi na upigaji wa wanawake katika kitongoji. Tunamuangalia Ally anaongoza watoto wanao ogopa kuchora.akifatia Pazi anawasaidia kuwachotea maji wazee mtu na mke wake, tuliona amekaa na mzee aliuliza maswali na yule mtu wakashirikishana vitu kwa mbali kijana mmoja hamjui.

Yote haya na hadithi nyingi inaonyesha ubora wa kila mshiriki, lakini vilevile gharama wanayolipa kwa kujitoa kwao katika kila siku ya maisha: Amini kwa kujitoa kwako hata kama unayoyafanya ni juu yako mwenyewe, kama alivyo fanya Eliza leo, alizunguka kwa vikundi 15 na vijana; lugha ya kejeri kama pazi pale anapo wasaidia wengine pasipo kuomba ujira “Kuto kumuacha mtu nyuma”.

Kila mmoja wakiwemo kundi la wawezeshaji, wamejifunza vitu vingi vinaweza kuwatia moyo katika utendaji wetu. Asante kwa nguvu zote, akili vitendea kazi, vilitia moyo na vijana walijitoa, sasa kuna haja ya kuangalia matumaini kwa siku za baadae.

**Romy Hoffmann**
**ATD Kimataifa**



## Kinacho jili hivi karibuni

- **Elimu Kwa Wote: Ripoti ya Utafiti na Mkutano na Walimu Wakuu wa Kinondoni**
- **Hivi karibuni utatangazwa Uongozi mpya wa timu ya ATD Kimataifa**
- **Ufunguzi wa ukurasa wa Facebook wa Vijana Marafiki wa ATD**

**Unaweza kuwasiliana na sisi !**

ATD Dunia ya Nne – S.L.P 61786 - Dar es Salaam
Email : atd.tanzania@gmail.com
Website: www.atd-fourthworld.org/where-we-are/africa/tanzania

ATD DUNIA YA NNE TANZANIA *JARIDA*

Aprili 2016

ATD FOURTH WORLD

Popote pale wanaume na wanawake wanapohukumiwa kuishi katika hali ya umaskini uliokithiri, haki za binadamu zimekiukwa. Kuja pamoja kuhakikisha kwamba hizi haki zinaheshimiwa ni jukumu letu makini.
- Joseph Wresinski (1917-1988) mwanzilishi wa ATD Dunia ya Nne

## Tahariri

***Kujifunza na kutenda kwa pamoja ili kuwa marafiki bora kwa asiyekuwa na rafiki***



Marafiki wapendwa

Ni matumaini yetu wote ni wazima wa afya, tunafuraha kuwajulisha juu ya hivi karibuni nini kilitokea katika harakati zetu za kila siku hapa ATD Dunia ya Nne Tanzania.

Mwezi wa tatu ATD iliandaa mkutano wa vijana. Vijana tofauti kutoka Tanzania, Kenya, Jamuhuri ya Demokrasia ya Kongo na Ethiopia, ambao ulifanyika Dar es Salaam kwa wiki moja. Miongoni mwetu si kila mmoja yupo imara, kama tutawaacha nyuma nyuma wale wote amabao hawako imara ni vipi wanaweza kwenda mbele bila ya sisi.

Lengo la mkutano lilikua ni kuwatia nguvu marafiki vijana wa ATD ambao tayari wanajitolea kufanya shughuli tofauti katika jamii zao katika njia ya kuwa pamoja na watu ambao hufikiriwa hawana marafiki katika jamii zetu.

Nilipata nafasi ya kujifunza kutoka kwa washiriki ni vipi wanajitoa na kujihusisha katika kuleta mabadiliko na matokeo chanya katika jamii zao, kama vile kuwa wote kitu kimoja na wale kufikiriana wenyewe. Hali hii huwawezesha kutengeneza jukwaa katika jamii kwa kila mmoja kuchangia mawazo kwa lengo la kuyashinda matatizo tukiwa kitu kimoja.

Namna pia wanavyopangilia mda kwasababu vijana walio wengi wa ATD ni wanafunzi na baadhi yao wanashughuli binafsi za kufanya, lakini bado wanajitolea mda wao kwa ajili ya watu ambao kila wakati wanapitia matatizo. Kupitia shughuli zao wanazozifanya wanaweza kutengeneza mahusiano miongoni mwao kama wanajamii. Niliona namna vijana ambavyo wapo tayari kila wakati kuwa pamoja na watu walio maskini mno kwa kipindi kirefu zaidi cha miezi na miaka ili kuendeleza uaminifu uliopo na kwenda mbele zaidi hatua kwa hatua kwa pamoja.

Hemed [ATD Mwanaharakati wa Kujitolea]



**Maktaba Maalum ya mMtaa Tandale. Watu kutoka Kongo, Kenya walikutana na walikuwa na wakati wa urafiki kabla ya kuanza semina.**



**Fabienne (Kiongozi kutoka Kanda ya Afrika)**

Tangu 20 hadi 25 March 2016, jumla ya vijana thelathini, kutoka Kenya, Tanzania, Ethiopia na Jamuhuri ya Demokrasia ya Kongo walikutana Dar es Salaam, Tanzania. Hii ni mara ya kwanza tukio la ATD kimataifa kwa Tanzania tangu Harakati zizaliwe hapa nchini. Lengo kuu lilikuwa ni kuimarisha ahadi za vijana kuchukua hatua katika jamii zao na kuongeza shauku ya vijana hai ambao huendelea kufanya kazi pamoja nao na ushupavu wa kuweza kufanya mapendekezo.

Harakati zetu hupata uimara wake katika dhamira ya kila mmoja wetu na kutuleta pamoja ili kushirikishana imani zetu, mashaka yetu na shauku ni muhimu kuvumilia...

Lengo kuu lilikuwa ni kuimarisha ahadi wanazo chukua watu ndani ya jamii zao na kuongeza shauku ya vijana hai kwamba inaleta nguvu ya kufanya mapendekezo.

Mapendekezo kutoka kwa washiriki mwisho wa kipindi: *“Mafanikio yoyote au maendeleo ya ulimwengu yapo mikononi mwetu sisi vijana: pale ulimwengu utakapo kuwa hakuna ubaguzi, ulimwengu pasipokuwa na umaskini. Lakini tu tunaweza kufanya kama tutaungana, huu mkutano hapa Dar es Salaam hautakuwa na mafanikio. Nilijifunza kuhusika kwa kupitia matatizo ya wengine, matatizo yale ya wengine, ni matatizo yangu na nina haki ya kumsaidia kwa kupata. Kutokana na haya tunakuwa rafiki wa wasiona rafiki”.*

(endalea...)

(…)

Semina hii iliwapa washiriki wote uhakika kwamba wanachokifanya ni kikubwa, siyo burudani na wao walipewa uhakika na fahari kwamba "Kile kidogo ambacho kila mtu anafanya kitakuwa kitu kikubwa". Kuwa rafiki wa asiyekuwa na rafiki, haya ni mafanikio ya kweli, na mafanikio haya husaidia kujenga amani.

Mara nyingi tunajadiliana juu ya 'kundi la-viongozi' au 'waandaaji-shughuli', lakini kikao hiki na mabadilishano yake yametuonyesha kwamba maneno haya hayatoshelezi. Wale ambao wanashiriki kuwa rafiki wa asiyekuwa na rafiki ni 'washiriki wa maarifa', watu ambao huunganisha jamii, 'wajenzi wa amani', makaka na madada wakubwa ambao huonyesha watoto njia ya maisha bora ya baadaye. Kwa upande wetu, Timu ya Kanda ya Afrika, ni chanzo cha fahari kubwa na msukumo wa kuona ahadi hizi.



**Matendo yetu hukamata mawazo ya vijana wengi na tunataka wengine wafuate muongozo wetu.**

Nimeacha nguvu kubwa na uangalifu wa yale muhimu ya kujitoa kwetu kwenye jamii. Naelewa thamani ya kujitoa kwetu. Shuhuda ya pazi aliyoelezea. Hii ilinifanya mimi nirudi nyuma na kuamua kusaidia wazee na majirani zangu (mke na mume) waliodharauliwa. Hawana makazi, wanaishi kwenye majengo wanayojenga wajenzi, wanachukuliwa na kukamatwa. Na sasa jengo limesha kwisha mwenyewe anataka nyumba yake. Hivyo wanatazamia kuondoka wana mfadhaiko. Muda mwingi huwa nakula nao chakula changu cha mchana. Wameshakuwa rafiki zangu.

Shuhuda za vijana wote ziliwakilishwa kwenye mkutano ulinifanya mimi kuwa na ndoto. Na nina ujasili na siku moja vijana wote wa Afrika watakutana kwa wito wa Joseph. Utendaji wetu umekamata kusudiio la vijana wengi na tuna tumaini wengine watafuata na utangulizi wetu. Ndio maana tumefungua kundi la Whatsapp. litatufanya kuungana na kuendelea kubadilishana. Tukirejea juu ya uwezekano vilevile kwenye kundi la Facebook. Kwahiyo tutaendelea kuwasiliana juu ya tunayo yafanya.

Christian (Kongo)

**Kutokana na semina hii nimepata imani kuwa ni muhimu sana, kuwa rafiki kwa asiyekuwa na rafiki.**

Familia yangu walifurahi kuniona. Niliporudi nyumbani kutoka kwenye semina. Ugumu ulikuwa kwa majirani, kweli wao walitegemea nimekuja na kitu chochote mfukoni, walisema lazima una kitu, hata kwa kutununulia soda.

Pale nilipo wambia 'sina' waliniambia umepoteza muda wako kama umeweza kurudi mikono mitupu. Katika jamii, inapokuwa mara ya kwanza kusaidia jamii katka mahitaji, watu wengine huuliza ni ndugu zako, kwa nini unakuwa wakwanza, kwanini umeguswa zaidi ya wengine. Baadhi ya watu wanajaribu kukuvunja moyo, Nina nguzo, Natumia uimara, moyo na ufahamu wangu.

Siwasikilizi wale wanao jaribu kunivunja moyo wale wote wanaojitoa wenyewe. Nitaendelea kusaidia marafiki zangu ambao hawana marafiki. Nitawaambia marafiki kuwa haya ni matunda ya Vijana wa ATD.Kutokana na hii semina nimeona ushawishi kuwa kuna umuhimu, kuwa na rafiki wasio na rafiki. Tunaposema hawa watu watajisikia wananguvu kwa ushawishi wa usemi huu, imechukuliwa kama kitu cha makini, ushawishi huu kwangu mimi umeenda kwa undani..




Oscar (Tanzania)






Wakati wewe unafanya mtu atambue kitu ni maendeleo. Mateso ya watu maskini sana yanaweza kupunguzwa wakati wa kuungana nao. Katika jamii yangu mimi usaidia kuwachotea maji wanandoa wa zamani, siyo tu kuwasaidia lakini pia kwa wao kuona jamii inawajali.   Pazi (Tanzania)



Nilivutiwa sana katika hadithi kutoka senegali na watu wanavyofanya kazi pamoja kwa kutengeneza mifereji ya maji katika maeneo yalioingiliwa na mafuriko. Wanashirikishana ujuzi jinsi ya kuyafanya maeneo safi na salama, hatimae kila mtu anafuraha. Kwa pamoja vijana kutoka nchi nyingine tuliungana, kama vijana tunapo kaa pamoja tunatengeneza kitu upendo. Hii inatuwezesha sisi vijana kufanya zaidi vile tulivyo vitarajia.   Ally (Tanzania)



Nilivutiwa na hadithi kutoka kwa vijana kutoka DR Congo, Kulikuwa na mtu ambaye ni mgonjwa, njia ya vijana kumsaidia mtu huyu ilikuwa kama yeye alikuwa jamaa yao na mtu huyu afya yake iliboreka na akawa mzima. Semina hii ilimarisha kufanya mambo bila kujali watu wanasema nini kama unajua uko sahihi.   Alfredi (Tanzania)

**Kuwa rafiki kwa asiyekuwa na rafiki si jukumu la mtu binafsi ila ni wajibu.**

Nilibahatika kuhudhulia Semina ya Vijana ilioandaliwa na Harakati za ATD Dar es Salaam. Katika maisha yangu sijawahi kupata uzowefu kama huu. Tulitembelea jamii ya Tandale, pale kuna baadhi ya vijana wamejitoa kabisa katika Maktaba ya Mtaa. Watoto wanahali ya kutaka kujifunza. Niliondoka na niliona jinsi gani vijana walivyohamasika kuishi katika roho ya Joseph Wresinski ambae alisema kufikiri na kujua ni vitendo ambavyo wanadamu wote wanafanya vyovyote katika maisha yaliyotolewa. Nilichokuwa nacho ni ujuzi nilioupata kutoka Chuo kikuu na nitakuwa na furaha kama nitawashirikisha watoto.

Kuwa rafiki kwa asiyekuwa na rafiki si jukumu la mtu mmoja bali ni jukumu letu sote. Kudumu na thamani zaidi milele kama vijana ninyi kamwe hatokuwa na uwezo wa kuwapa jamii dhamira yenu. Jaribu kadri iwezekanavyo ili kuwa rafiki na wale walio pembezoni, hawana haja ya fedha zenu bali kukubalika kama binadamu.

Kwenye jamii yangu, nilikuwa nawapa changamoto ya kulazimika kufanya kuwa na furaha na kupunguza mateso ya watoto wetu. Niliamua kuwa njia kwa kupitia mchango wangu kuwa bariki watoto. Watoto wana tuhitaji sisi. Elimu itawawezesha lakini kitakacho wafanya wawe bora ni ubinadamu wa upendo wetu, kuwajali na kuwa tayari.

Tumekuwa na upendo mmoja lakini umegawanyika kwa tamaa. Tufanye maamuzi kuwa na kidogo kwa kila mtu atosheke, usijiwekee kumiliki lakini kuchangia ni uhalisi tosha wa uwepo wako.

Patrick (Kenya)



## Washiriki walikuja kutoka…

- **Marafiki Vijana wa ATD Tanzania**
- **Kundi la Vijana wa ATD Kongo (Bukavu, Goma and Uvira)**
- **Kambi ya Edmund Rice Kibera (Nairobi, Kenya)**
- **Tushirikiane (Kenya)**
- **Pomoja (Ethiopia)**